**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/WZ/2024/08**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000223**

**KATI YA**

**ADAM MTUNDA KAOMBWE ........................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) .......................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 12 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 12 mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) (Mlalamikiwa) aunganishe huduma ya umeme kama ambavyo Mlalamikaji ameomba kwa mujibu wa mkataba wa huduma kwa wateja. Mlalamikaji ni mkazi wa Kijiji cha Igigwa Barazani, Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora. na anaeleza kwamba, mnamo mwezi Septemba 2023 alifanya maombi ya kuunganishiwa huduma ya umeme na kupewa namba ya maombi 200923-1334 lakini hakuweza kupata huduma hiyo mpaka kufikia sasa. Mlalamikaji alifanya jitihada mbalimbali za kufika ofisini kwa Mlalamikiwa kufuatilia maombi yake lakini hakufanikiwa kupata huduma.

Ndipo alipoamua kuwasilisha malalamiko yake ofisi za EWURA CCC Mkoa wa Tabora, ambao walimwelekeza ajaze fomu na kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka (EWURA). Mnamo tarehe 1 Oktoba 2024, ofisi Kanda ya Magharibi ilipokea rasmi malalamiko ya Bw. Adam Kaombwe (Mlalamikaji).

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 10 mwezi Oktoba mwaka 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 25 Oktoba 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea maombi ya Mlalamikaji na kueleza kwamba Mlalamikaji alipatiwa namba ya maombi 200923-1334 na kwamba mnamo tarehe 2 Oktoba 2023, fundi kutoka ofisi yake alifika eneo la Mlalamikaji na kugundua kuwa inahitajika mashine umba (*Transformer*) nyingine yenye nguvu zaidi itakayoweza kukidhi mahitaji ya umeme kwa wakazi wa eneo hilo akiwemo Mlalamikaji. Ilipofika tarehe 16 mwezi wa Februari 2024, walimjulisha mkandarasi wa Mlalamikaji kwa ujumbe kuwa hawataweza kutekeleza ombi la maunganisho mapya kutokana na uhitaji wa mashine umba (*Transformer*) yenye ukubwa wa kukidhi mahitaji, jambo ambalo linahitaji fedha nyingi ambayo kwa sasa Mlalamikiwa hana bajeti hiyo. Mlalamikiwa anaeleza kuwa alimtaka Mlalamikaji kusubiri hadi pale atakapopata fedha za kubadilisha mashine-umba ndipo atampatia huduma ya umeme.

Baada ya kupokea utetezi huo, Mamlaka (EWURA) ilipanga kikao cha usuluhishi ambacho kilifanyika tarehe 31 Disemba 2024, wilayani Sikonge ambapo Wadaawa walikubaliana kusuluhisha mgogoro nje ya kikao cha usuluhishi na hivyo wapewe muda wa wiki moja. Ilipofika tarehe 1 Januari 2025, Mlalamikiwa alitoa taarifa kwa njia ya simu kwamba tayari ameshaunganisha huduma ya umeme kwa Mlalamikaji kama alivyokuwa ameomba. Kwa upande wake Mlalamikaji alitoa taarifa kwamba bado anahitaji mkandarasi wake aingize umeme ndani na hivyo atakapokamilisha zoezi hilo ataijulisha Mamlaka. Mnamo tarehe 22 Januari 2025, Mlalamikaji aliijulisha Mamlaka kwa njia ya ujumbe wa simu kwamba Mlalamikiwa ameunganisha huduma ya umeme na hivyo hana nia ya kuendelea na malalamiko na anaomba kuyaondoa.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 12 mwezi Februari 2025.

..............................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**